# OFISI YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKARI ZA MITAA
## HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE


**SHULE YA SEKONDARI IKUTI,**
**S. L. P 141,**
**TUKUYU.**
**TAREHE ....................**
**MOB: 0755777754**


**KUMB;NA HRS/IKSS/S.1082/JI/2021**

**KWA……………………………………………..**

**…………………………………………….....**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IKUTI ILIYOKO WILAYA YA RUNGWE MKOA WA MBEYA MWAKA 2021.**

**1.0 UTANGULIZI**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari Ikuti iko umbali wa kilomita 3 kutoka kwenye mji mdogo wa Ikuti. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11/01/2021 siku ya jumatatu. Unatakiwa kuripoti shuleni siku ya kufungua shule tarehe 11/01/2021 saa moja kamili asubuhi. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 18./01/2021.

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.1 SARE ZA SHULE**

**(a) MAHITAJI YA SARE KWA WANAFUNZI WA KIUME NIKAMA IFUATAVYO:-**

i) Suruali mbili moja rangi nyeusi na nyingine damu yam zee zenye upana wa kutosha na urefu wakutosha na ziwe na upindo (turn – up) na marinda mawili kila upande.

ii) Mashati mawili meupe ya kitambaa cha tetron mikono mifupi

iii) Soksi nyeusi jozi mbili

iv) Viatu vyeusi vya ngozi kisigino kifupi jozi mbili vya kamba

v) Tai mbili za rangi ya suruali (moja nyeusi na nyingine ya damu yam zee)

vi) Nguo za michezo, fulana moja rangi ya bluu, bukta moja ya rangi nyeusi na raba

vii) Mkanda mweusi wa ngozi

viii) Sweta ya rangi ya bluu

**(b) MAHITAJI YA SARE KWA WANAFUNZI WA KIKE NIKAMA IFUATAVYO:-**

i) Sketi mbili moja rangi nyeusi na nyingine damu yam zee zenye upana wa kutosha na urefu unaofika kwenye ankle ya miguu. Sketi ziwe na rinda moja pana mbele na nyuma na mengine madogomadogo.

ii) Mashati mawili meupe yakitambaa cha tetron mikono mifupi
iii) Soksi nyeupe jozi mbili
iv) Viatu vyeusi vya ngozi kisigino kifupi jozi mbili vya kamba
v) Tai mbili za rangi ya sketi (moja nyeusi na nyingine damu yam zee)
vi) Nguo za michezo; fulana moja rangi ya bluu, tracksut moja ya rangi nyeusi na raba
vii) Sweta ya rangi ya bluu

**2.2 MAHITAJI YA DARASANI**

i) Daftari kubwa kumi na mbili (counter booksthree quire)
ii) Kalamu za wino zakutosha
iii) Rula ndefu ya sm 30
iv) Kalamu za risasi za kutosha
v) Mkebe (mathematical set) ulio na vifaa vyote
vi) Mfuko mzuri wa kubebea daftari (school bag). Mifuko ya Rambo hairuhusiwi inaharibu mazingira.
vii) Dictionary.
viii) Picha nne zenye ukubwa wa passport zilizopigwa kwenye background ya bluu bahari
ix) Mzazi unashauliwa kumnunulia vitabu vinavyotumika katika shule za sekondari ili aweze kujisomea awapo nyumbani

**2.3 CHAKULA KWA WANAFUNZI WA KUTWA**

Niwajibu wa mzazi kuhakikisha kuwa mtoto wake anapata chakula awapo shuleni ili aweze kujifunza vizuri. Gharama za chakula na fedha za kuwalipa wapishi zitapangwa na kujadiliwa na wazazi katika kikao kitakachounda kamati ya chakula.

**3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama Ilivyorekebishwa kwa sheria na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo Yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya RAIS yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

**3.1 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sale ya shule wakati wote unapotakiwa.

h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
i) Kutunza mali za umma.

**3.2. MAKOSA YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI SHULE.**

a) Wizi
b) Uasherati na Ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, Cocaine, Mirungi, Kubeli nakadhalika.
e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g) Kudharau Bendela ya Taifa.
h) Kuwa mjamzito/kupata mimba.
i) Kuoa au kuolewa.
j) Kutoa mimba.
k) Kugoma/kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule na watu.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi
m) Kuwa na simu ya mkononi

**4.0 MAMBO MENGINE YA MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI.**

a) Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hiyo itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi ya kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kwa makini.**

**KARIBU SANA IKUTI SEKONDARI**

**……………………….**

**VERDIANA E. MATERU**

**MKUU WA SHULE.**

# OFISI YA RAIS

# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
# HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE
# SHULE YA SEKONDARI IKUTI

## A. TAARIFA YA MWANAFUNZI

Jina la ukoo ______________________________________________________________.

Jina la kwanza ____________________________________________________________.

Jina la kati kama lipo kwenye vyeti ____________________________________________.

Jinsi _______ tarehe ya kuzaliwa ______________________________________________.

Mahali ulipozaliwa kijiji/ Mtaa _______________________ Kata ________________ Wilaya ya Mkoa wa ______________________Namba ya usajili ________________ Mwaka wa masomo Hadi _______________________.

## B. AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi ________________________________________________________naahidi kuwa sitashiriki/ nitashiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai katika kipindi chote cha masomo.

Tarehe _________________ Jina _________________ Sahihi ________________.

## C. SEHEMU HII IJAZWE NA MZAZI AU MLEZI WA MWANAFUNZI.

Mimi ______________________________________________ambaye ni mzazi au mlezi wa mwanafunzi ___________________________________________________ ambaye amechaguliwa kujiunga na Elimu ya sekondari mwaka 2021 katika shule ya sekondari Ikuti nakubaliana na sheria, kanuni, kumpatia mahitaji yote ya muhimu na kukubaliana na maelekeo mengine yatakayotolewa na shule.

Sahihi ya mzazi/ mlezi ___________________Tarehe ___ Mwezi ___ Mwaka _____.

**NB: Karatasi hii irudishwe shuleni baada ya kujazwa**.

**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**RUNGWE DISTRICT COUNCIL**

IKUTI SECONDARY SCHOOL,
P. O BOX 141,
TUKUYU.

TO.

MEDICAL OFFICER,

...................................................

..................................................

...................................................

Please examine

.........................................................................................................................................................

As to him / her fitness for pursuing further education in this school.

1. Heamoglobin.........................................................................................................................................

2. P. v. bleeding.......................................................................................................................................

3. Sight.....................................................................................................................................................

4. Blood pressure...................................................................................................................................

5. Urine for sugar and pregnancy tests..........................................................................................

6. Stool routine examination.............................................................................................................

7. Asthma...................................................................................................................................................

8. Skin diseases......................................................................................................................................

9. Leprosy..................................................................................................................................................

10. Epilepsy...............................................................................................................................................

11. Pulmonary tuberculosis................................................................................................................

12. Deformity............................................................................................................................................

13. Mental problem................................................................................................................................

14. Comments...........................................................................................................................................

Sign.............................

Official stamp.

# TAARIFA BINAFSI

1. **Jina kamili la mwanafunzi ____________________________________________________.**

2. **Jina kamili la mzazi __________________________________________________________.**

   **Anuani kamili** _____________________________________________________________.

   ___________________________________________________________________________.

   ___________________________________________________________________________.

   Namba ya simu ___________________________________________________________.

   Mkoa________________________________________.

3. Majina ya watu watatu ambao mawasiliano ya kiofisi kuhusu mwanafunzihusika yatafanyika.

| | JINA | UHUSIANO | NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|---|
| i. | ……………………………………… | ……………… | …………..…… |
| ii. | …………………………….……… | ……………… | …………..…… |
| iii. | …………………………….………. | ………………. | ……………..…… |

4. Jina sahihi la mzazi au mlezi ……….…………………………… sahihi ……………

5. Jina kamili la afisa mtendaji ……………..………………………. Sahihi …………..

6. Taarifa hii irudishwe kwa mkuu wa shule ya sekondari Ikuti.

_____________.

V. E. MATERU

MKUU WA SHULE

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE**

**Simu: 0755777754**
**KUMB;NA HRS/IKSS/S.1082/JI/202**

**SHULE YA SEKONDARI IKUTI,**
**S. L. P 141,**
**TUKUYU.**

**Tarehe ______________________.**

===============================================================

ANUANI YA MZAZI AU MLEZI,

_________________________,

______________________,

________________.

TAREHE ___________________.

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI IKUTI,
S. L. P 141,
TUKUYU.

**YAH: HATI YA KUKUBALI MASHARTI KUHUSU MTOTO WANGU KUSOMA SEKONDARI YA IKUTI.**

Mimi ______________________________________________________mzazi au mlezi wa mwanafunzi __________________________________________________Aliyekuwa akisoma shule ya msingi ___________________________Katika wilaya ya ___________________ ninakubali mtoto wangu asome shule ya sekondari Ikuti iliyopo wilaya ya Rungwe kwa kufuata masharti yafuatayo.

1. Kwamba mtoto wangu atahudhuria masomo kama kawaida kufanya shughuli nyingine zote za shule tangu kidato cha kwanza mpaka cha nne, na atazingatia sheria na taratibu zote za shule.
2. Nakubali masharti na gharama zitakazotolewa katika barua ya kuitwa kwa mwanafunzi (joining instructions) na nitayatimiza kwa wakati unaotakiwa.
3. Nitahakikisha atafika shuleni kwa kufuata tarehe zilizopangwa kwa kipindi chote cha miaka minne.

**__________________.** **__________________________.**

**TAREHE** **SAINI YA MZAZI / MLEZI**